Habarileo Jumapili Aprili 12, 2026 Pg 3

# Wamiliki wa mabasi, daladala wasitisha mgomo leo

Na Ikunda Erick

UMOJA wa Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) kwa kushirikiana na Umoja wa Wasafirishaji Abiria Dar es Salaam (UWAMADAR) umetangaza kusitisha mpango wa mgomo uliokuwa uanze leo, na badala yake umewataka wamiliki kuendelea kutoa huduma ya usafiri kwa wananchi, huku wakisubiri majibu ya serikali.

Walisema wanasitisha mgomo huo baada ya serikali kusikia kilio chao cha kupanda kwa bei ya mafuta na kumtuma Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa kuzungumza nao na kuwahakikishia mapendekezo yao yanafanyiwa kazi ndani ya muda mfupi. Akizungumza Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Uwamadar, Kismat Jaffer alisema wamefanya kikao jana (juzi) na Profesa Mbarawa na wamekubaliana kuwa wadau wa usafirishaji kuipa serikali muda wa kufanyia kazi malalamiko yao.

"Tumefanya mazungumzo na waziri na tumeahidiwa kuwa matatizo yetu yatafanyiwa kazi. Hivyo, tunaendelea kutoa huduma, badala ya kuingia kwenye mgomo wakati tukisubiri majibu," alisema Jaffer.

Alisisitiza kuwa wamiliki wa daladala wanapaswa kuzingatia viwango halali vya nauli vilivyowekwa, akieleza kuwa ni muhimu kufuata utaratibu uliopo huku suluhisho la kudumu likisubiriwa kutoka serikalini.

"Tunaomba wamiliki wa daladala tuendelee kutoa huduma, tusiache kwa maana itatafsiriwa ni mgomo na tukifanya hivyo si sawa, kwa sababu serikali imekuja kuzungumza na sisi basi tuipe muda wa kutujibu wakati huo huduma zikiendelea. Atakayekiuka ni yeye ila sisi msisitizo wetu tuendelee kutoa huduma," alisema Jaffer.

Kwa upande wake, Katibu wa Taboa, Priscus Joseph alisema awali walipanga kusitisha huduma kuanzia Aprili 12 (leo), lakini baada ya mazungumzo na serikali, wameona ni busara kuendelea kutoa huduma ili kuepusha athari kwa abiria.

"Serikali imetuhakikishia kuwa itashughulikia changamoto zetu ndani ya muda mfupi. Tunawaomba wanachama wetu waendelee kutoa huduma kama kawaida," alisema Joseph.

Awali, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) iliwataka wadau wa sekta hiyo kuendelea kuwa watulivu, huku ikiendelea kuchakata maoni yao yaliyowasilishwa Aprili 8, mwaka huu kwenye mkutano wadau hao kuhusu mapendekezo ya kupandisha nauli.

Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Dk Habibu Suluo alisema ni kosa kisheria kwa watoa huduma kugoma na kusisitiza kuwa hatua kali, ikiwemo kufutiwa leseni zinaweza kuchukuliwa dhidi ya watakaokiuka sheria.

Awali, wadau wa usafirishaji walidai kupanda kwa bei ya mafuta kumeathiri uendeshaji wa huduma zao, hali iliyowalazimu kuomba mapitio ya nauli ili kuendana na gharama za uendeshaji.

Hata hivyo, Latra imewapa wadau muda wa ziada wa siku 14 kuwasilisha mapendekezo yao kabla ya kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu iwapo nauli zitapandishwa au la.

CamScanner